

JINA _____ DARASA _____

SAHIHI _____ TAREHE _____

102/3

KISWAHILI

KIDATO CHA TATU

MUDA: 2:30

MAAGIZO

- i) JIBU MASWALI MANNE PEKEE
- ii) SWALI LA KWANZA NI LA LAZIMA
- iii) CHAGUA MASWALI HAYO MENGINE MATATU KUTOKA KWA SEHEMU NNE ZILIZOBAKIA (RIWAYA, TAMTHILIA, HADITHI FUPI NA FASIHI SIMULIZI)
- iv) USIJIBU MASWALI MAWILI YA KITABU KIMOJA

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|--------------|-----------|-------|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| 5 | 20 | |
| 6 | 20 | |
| 7 | 20 | |
| 8 | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

1.LAZIMA-USHAIRI

SOMA SHAIRI LIFUATALO KISHA UJIBU MASWALI YATAKAYOFUATA

Natunga nikiwaasa, msije kujijutia,
Mitego sije wanasa, mkaja kuangamia,
Tamaa nyingi za pesa, gereza zitawatia
Kila mpenda rushuwa, jela inamkonyeza.

Jela inamkonyeza, kama hutajizuwia,
Haina ndugu gereza, jela si ya kuchezea,
Inajuvya na kupoza, wenye nguvu hutulia,
Kila mpenda rushuwa, jela inamkonyeza.

Rushuwa si kitu chema, walaji jihadharini,
Mkila zitawakwama, zitawatoka puani,
Wazilao hulalama, si mimi ila fulani,
Kila mpenda rushuwa, jela inamkonyeza.

Ridhika na upatacho, kama moja au mbili,
Usitaraji mkocho, apatao Bwana Ali
Tamaa zako za macho, zitakuletea mbuli,
Kila mpenda rushuwa, jela inamkonyeza.

Nimeona kemu kemu, wenye vyeo kutumia,
Maleba wakiwahimu, rushuwa kuwaletea,
Muogopeni Karimu, Leba haombwi rushua,
Kila mpenda rushuwa, jela inamkonyeza.

Kuna wengi mahakimu, haki wanazipinduwa,
Yatima kuwadhulumu. kwa kupapia rushuwa,
Kwa kutaka darahimu, aso haki anapewa,
Kila mpenda rushuwa, jela inamkonyeza.

MASWALI

- Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 1)
- Mshairi anatoa tahadhari gani katika shairi hili? (alama 1)
- Shairi hili ni la bahari gani? Toa sababu. (alama 3)
- Eleza toni ya nafsineni. (alama 2)
- Onyesha jinsi idhini ya mshairi ilivyotumika katika shairi hili. (alama 3)
- Eleza muundo wa shairi hili. (alalama 4)

- g) Onyesha jinsi kanuni za kiarudhi zilivyozingatiwa) (alama 2)
- h) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari. (alama 4)

SEHEMU B:RIWAYA

KIDAGAA KIMEMWOZEA –KEN WALIBORA

2.Vijana wana mchango muhimu katika kuleta mabadiliko. Thibitisha kauli hili ukirejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

AU

3."Kulea mimba si kazi, kazi ni kulea mwana."

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Taja na kuthibitisha mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)
- c) Eleza mifano mingine inayothibitisha kutowajibika kwa taasisi inayorejelewa na dondoo hili.(alama 4)
- d)i) Jadili sifa tano za Mtemi Nasaba Bora. (alama 5)
- ii) Onyesha umuhimu wa mhusika huyu. (alama 5)

SEHEMU C: TAMTHILIA

KIGOGO-PAULINE KEA

4.Fafanua jinsi mbinu ya kinaya ilivyotumiwa katika tamthilia ya Kigogo. (alama 20)

AU

5. "Ha-ha-ha-ha! Profesa wa siasa na historia ashasema."

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Taja na utolee mifano mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)
- c) Jadili mbinu mbalimbali ambazo viongozi katika tamthilia ya Kigogo wanatumia ili kujidumisha mamlakani. (alama 12)

SEHEMU D:FASIHI SIMULIZI

6)a) Jadili mambo ambayo hufanikisha uwasilishaji wa fasihi simulizi. (alama 10)

b) Eleza changamoto zinazukabili uendelezaji wa fasihi simulizi. (alama 10)

AU

7a) Eleza dhima ya masimulizi ya hadithi.(alama 5)

b) Hadithi zilitambwa wakati gani? Eleza sababu za hadithi kutambwa wakati uliotaja (alama5

c) Taja aina nne za hadithi na uzitolee ufafanuzi mwafaka. (alama 4)

d)i) Taja fomula ya ufunguzi wa hadithi. (alama 1)

ii) Eleza umuhimu wa fomula hii. (alama 5)

SEHEMU E:HADITHI FUPI

TUMBO LISILOSHIBA-ALIFA CHOKOCHO NA DUMU KAYANDA

8.Jadili ufaafu wa anwani “Tumbo Lisiloshiba” kwa hadithi hii. (alama 20)

for free revision past papers visit: www.freekcsesastpapers.com